



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

MWALIKO WA WATAZAMAJI WA UCHAGUZI MDOGO WA
UBUNGE KATIKA MAJIMBO YA KOROGWE VIJIJINI, UKONGA,
MONDULI NA MADIWANI KATIKA KATA 23 KWENYE
HALMASHAURI 15 ZA TANZANIA BARA

Kwa mujibu wa kifungu cha 46 (2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 48 (2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Madiwani), Sura ya 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuendesha Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Majimbo matatu ya Korogwe Vijijini, Ukonga na Monduli, na Madiwani katika Kata 23 zilizopo katika Halmashauri 15 za Tanzania Bara.

Kwa ajili ya kuweka uwazi katika Uchaguzi huo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia Kanuni ya 18 (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2015, na Kanuni ya 14 (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2015, inapenda kualika Asasi za Kiraia na Taasisi mbalimbali za ndani zinazotaka kuwa Watazamaji wa Uchaguzi katika Uchaguzi Mdogo unaotarajiwa kufanyika tarehe **16 Septemba, 2018**.

Majimbo yatakayofanya Uchaguzi mdogo ni:

Na.	MKOA	HALMASHAURI	JIMBO
1.	Arusha	Halmashauri ya Wilaya ya Monduli	Monduli
2.	Dar es Salaama	Halmashauri ya Manispaa ya Ilala	Ukonga
3.	Tanga	Halmashauri Wilaya ya Korogwe	Korogwe Vijijini

Kata (23) katika Halmashauri 15 za Tanzania Bara.

NA.	MKOA	HALMASHAURI		KATA
1.	ARUSHA	Halmashauri ya Wilaya ya Arusha	1	Kiutu
			2	Olturoto
		Halmashauri ya Wilaya ya Monduli	3	Mswakini
2	DAR ES SALAAM	Halmashauri ya Manispaa ya Ilala	4	Zingiziwa
			5	Vingunguti
		Halmashauri ya Manispaa ya Temeke	6	Mbagala Kuu
3	DODOMA	Halmashauri ya Jiji la Dodoma	7	Kizota
4	GEITA	Halmashauri ya Wilaya ya Geita	8	Bugalama
5	KILIMANJARO	Halmashauri ya Wilaya ya Hai	9	Machame Uroki
			10	Kia
		Halmashauri ya Wilaya ya Siha	11	Nasai
6	KAGERA	Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi	12	Kashenye
7	MANYARA	Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto	13	Loorela
8	MBEYA	Halmashauri ya Jiji la Mbeya	14	Maanga
			15	Sisimba
			16	Iwambi
			17	Nsalaga
		Halmashauri ya Wilaya ya Kyela	18	Nkuyu
9	SIMIYU	Halmashauri ya Wilaya ya Meatu	19	Mwanhuzi
			20	Tindabuligi
			21	Kisesa
10	TANGA	Halmashauri ya Jiji la Tanga	22	Mwanzage
			Halmashauri ya Mji wa Korogwe	23

Asasi/Taasisi zinapaswa kuzingatia masharti yafuatayo wakati wa kuwasilisha maombi yao:


- i. Anuani kamili ya Asasi husika,
- ii. Anuani ya Makazi ya Ofisi ya Taasisi husika ilipo,
- iii. Mahali/sehemu ambapo Taasisi husika inafanyia kazi,
- iv. Shughuli ambazo zinafanywa na Taasisi husika kwa mujibu wa Hati ya Usajili,
- v. Kutaja sehemu ambazo Asasi/Taasisi inataka kufanya zoezi hilo la Utazamaji
- vi. Kutaja idadi ya watu ambao Asasi/Taasisi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na taarifa zao.
- vii. Kutaja majina na namba za simu za viongozi wa Taasisi husika kama yalivyoandikwa katika Hati za Usajili wa Taasisi.
- viii. Ikiwa Taasisi inahusisha watendaji wa Kimataifa, wawili lazima wawe Watanzania.
- ix. Kuambatisha nakala/kivuli cha Hati ya Usajili wa Taasisi husika.
- x. Kuambatisha nakala/kivuli cha Katiba ya Taasisi/Asasi husika.

Aidha, Taasisi zitakazopewa vibali vya kuwa Watazamaji zitapaswa kuzingatia mwongozo kwa watazamaji wa ndani na wa kimataifa ulioandaliwa na Tume kwa mujibu wa Kanuni ya 24 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2015, na Kanuni ya 20 ya Kanuni za Uchaguzi wa Madiwani za mwaka 2015.

Maombi ya kuwa watazamaji wa Uchaguzi yatapaswa kuwasilishwa
Tume ya Taifa ya Uchaguzi Makao Makuu kuanzia tarehe 01 - 09
Septemba, 2018 kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Uchaguzi,
Tume ya Taifa ya Uchaguzi,
Posta House, Ghorofa ya 7,
Mtaa wa Ghana/Ohio,
S.L.P. 10923,
DAR ES SALAAM.

Imetolewa leo tarehe 20 Agosti, 2018



Salvius F. Nkwera

KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI